**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA RAISI**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**HALMASHAURI YA WILAYA YA MAKETE**

Simu Na: +255 (026) 2740016
Nukushi: +255 026 2740103
BaruaPepe: ded@makete.go.tz
Tovuti:http:www.maketedc.go.tz
***Unapojibu tafadhali taja;***
***Kumb. Na.*****JA.172/302/01/149**

Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji,
Halmashauri Wilaya ya Makete,
4 Barabara ya Bomani,
59582 MAKETE, NJOMBE,
**S.L.P 6, MAKETE**
**22/02/2023**

## TANGAZO LA NAFASI YA KAZI MLINZI (SECURITY GUARD)

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Makete anawatangazia nafasi sita (6) ya kazi ya Mlinzi (Security Guard) kwa Halmashauri ya Wilaya ya Makete.

### 1. SIFA ZINAZOHITAJIKA

- i. Awe Mtanzania
- ii. Awe na elimu ya kidato cha nne na kuendelea
- iii. Awe amehitimu kidato cha nne na kufuzu mafunzo ya Jeshi la Akiba, Polisi, JKT au mafunzo ya Zimamoto kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- iv. Waombaji wote wawe hawazidi miaka arobaini na tano (45) na hawapungui umri wa miaka kumi na nane (18)
- v. Asiwe na makosa ya jinai

### 2. MASHARTI YA AJIRA

- i. Ajira ya mkataba (miezi mitatu) “renewable”
- ii. Mshahara ni 200,000/= kwa mwezi

### 3. MAJUKUMU YA KAZI YA MLINZI (SECURITY GUARD)

- i. Kuhakikisha mali yoyote ya Ofisi inayotolewa langoni (Nje ya Ofisi) ina hati ya idhini.
- ii. Kuhakikisha mali yole inayoingizwa langoni inazo hati za uhalali wake.
- iii. Kulinda usalama wa majengo, Ofisi na mali za Ofisi mchana na usiku.
- iv. Kuhakikisha kwamba milango na madirisha yote yamefungwa ipasavyo mwisho wa saa za kazi.
- v. Kuhakikisha kwamba wageni wote wanaoingia katika eneo la Ofisi wanaidhini ya kufanya hivyo.

vi. Kupambana na majanga yote yatakayotokea katika sehemu ya kazi kama vile moto, mafuriko n.k na kutoa taarifa katika vyombo vinavyohusika, kama vile polisi na zimamoto.
vii. Kutoa ushauri wa jinsi ya kuboresha huduma ya ulinzi mahali pa kazi.

**UTARATIBU WA UOMBAJI:**

i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania na awe tayari kufanya kazi sehemu yoyote kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Makete
ii. Barua za maombi ziambatanishwe na nakala za vyeti vya elimu, Taaluma, Cheti eha kuzaliwa na picha mbili za rangi (Passport size)
iii. Waombaji wote wanatakiwa wawe na umri kuanzia 18 hadi umri usiozidi miaka 45.
iv. Waombaji waliokidhi sifa wataitwa kwenye usaili
v. Waombaji watakaoitwa kwenye usaili watatakiwa waje na vyeti halisi (original Certificate).
vi. Waombaji waandike anuani zao kwa usahihi na namba zao za simu.
vii. Wawe na wadhamini wawili (2) mmoja akiwa Mwenyekiti wa Kijiji na andike majina yao na nama za simu katika barua ya maombi.

**NB**: Maombi yanaweza kuandikwa kwa lugha ya Kiswahili au Kingereza na yatumwe kwa anwani ifuatayo:-

**Mkurugenzi Mtendaji ((W),**
**Halmashauri ya Wilaya ya Makete,**
**S.L.P. 6,**
**MAKETE.**

Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe **28/02/2023** saa **9:30 alasiri** na wale watakaokuwa wamekidhi vigezo na kuteuliwa wataitwa kwenye usaili.


William M. Makufwe
Mkurugenzi Mtendaji (W)
**Halmashauri ya Wilaya ya Makete**
MKURUGENZI MTENDAJI (W)
MAKETE

**Nakala:**

Meneja wa Redio
Redio Kitulo Fm
**MAKETE**

Mbao zote za Matangazo
Halmashauri ya Wilaya
**MAKETE**